**KUHAKIKISHA ULINZI**

**JUMUIYA YA ULAYA MWONGOZO WA WATETEAJI WA HAKI ZA BINADAMU**

## I. AZMA

1. Ufadhili wa ulinzi wa wateteaji wa haki za binadamu ni swala ambalo lilikwishaundwa kwa Jumuiya ya Ulaya kwa sera ya uhusiano wa mambo ya nje. Azma ya Miongozo huu ni kutoa mapendekezo dhati ya kuzidisha hatua ya EU kuambatana na jambo hili. Miongozo yaweza kutumiwa katika kuwasiliana na mataifa yanayoendelea katika viwango vyote pamoja na mikutano ya nchi zinazohusika katika kufadhili na kuimarisha mikakati ya jumuiya kwa kukuza na kuhimiza heshima ya haki ya kutetea haki za binadamu, miongo vile vile hutoa kuingilia kati kwa jumuiya katika hatari zinazowakabili wateteaji wa haki za binadamu na kupendekeza njia za kuwafadhili na kuwasaidia. Swala muhimu la miongozo ni ufadhili wa mpangilio maalum wa tume ya UN katika haki za binadamu pamoja na wakala maalum wa wateteaji wa haki za binadamu na njia mwafaka za utaratibu wa maeneo katika kuwalinda wateteaji wa haki za binadamu. Miongozo itasaidia misheni za nchi shiriki na wajumbe wa tume ya ulaya katika mtazamo wao wa wateteaji wa haki za binadamu. Huku shughuli zao bayana ni kuhusu wateteaji wa haki za binadamu ni jukumu lao ni azma yao ya kimsingi, Miongozo itachangia pia katika kuimarisha sera za haki za binadamu za EU kwa jumla.

## II. UFAFANUZI

2. Kwa azma ya kufafanua wateteaji wa haki za binadamu kwa Miongozi hii ya kutenda kazi aya ya 1 ya “Daimio la UN katika Haki na Jukumu la Watu Binafsi, Makundi na Vyombo vya Jamii kwa Kukuza na Kulinda Wateteaji wa Haki za Binadamu Wote Wanaotambulika na Msingi ya Uhuru” (tazama Kiambatisho cha I) ambayo yasema kwamba, “Kila mtu ana haki, kibinafsi na kushirikiana na wengine, katika kukuza na kujikakamua katika kutetea na kufikia haki za binadamu na misingi ya uhuru nchini na katika viwango vya kimataifa” hupatikana.

3. Wateteaji wa haki za binadamu ni watu binafsi, makundi na vyombo vya jamii ambavyo hukuza na kutetea haki za binadamu zinazotambulika kote na misingi ya uhuru. Wateteaji wa haki za binadamu hufuata ukuzaji na ulinzi wa umma na haki za kisiasa pamoja na ukuzaji, uteteaji na kufikia haki za kiuchumi, kijamii na zile za kitamaduni. Wateteaji wa haki za binadamu vile vile hukuza na hulinda wanachama wa makundi kama vile jamii za kiasili. Ufafanuzi haujumlishi wale watu binafsi au makundi ambayo hukiuka au hueneza dhuluma.

## III. UTANGULIZI

4. Muungano wa EU huunga mkono kanuni zilizomo kwenye Daimio juu ya Haki na wajibu wa Watu Binafsi, Makundi na Vyombo vya Umma katika Kueneza na Kulinda Haki za Binadamu zinazotambulika kote na Uhuru wa Kimsingi. Ingawaje wajibu wa kimsingi kwa kueneza na kulinda haki za binadamu huwa wa mataifa, muungano wa EU hutambua kwamba watu binafsi makundi na vyombo vya umma yote hutekeleza sehemu muhimu katika kuendeleza chanzo cha haki za binadamu. Kazi za wateteaji wa haki za binadamu ni pamoja na:

- uandishi wa dhuluma;
- kutafuta suluhisho kwa wadhirika wa dhuluma kama hizo kwa kutoa huduma za kisheria, kisaikolojia, kimatibabu na ufadhili mwingineo na;
- kupambana na tamaduni za kuepuka adhabu ambazo hutumikia mifumo ya kukeuka haki za binadamu mara kwa mara na uhuru wa kimsingi.

5. Kazi za wateteaji wa uhuru uhusika katika kusoa sera za serikali na vitendo. Hata hivyo, serikali isichukulie jambo hili kuwa kinyume. Sera za kuruhusu nafasi ya uhuru wa mawazo na mijadala huru juu ya serikali na vitendo vyake na muhimu na njia iliyojaribuwa kwa kuanzisha viwango mwafaka vya kulinda haki za binadamu. Katika mojawapo ya sehemu za mashauri zinaweza kutekeleza wajibu muhimu kwa kuandika kielelezo mwafaka cha sheria na pia katika kusaidia kutafuta mipango ya kitaifa na njia juu ya haki za binadamu. Jukumu hili pia ni lazima litambuliwe na kuungwa mkono.

6. Muungano wa EU hutambua kwamba kazi za Wateteaji wa Haki za Binadamu zimetambuliwa zaidi katika miaka kadhaa imepita. Kazi hizi zimeendelea kuhakikisha uteteaji zaidi wa waadhirika wa dhuluma. Hata hivyo, mafanikio haya yamepatika kwa kujitolea muhanga (gharama ya juu sana): wateteaji wenyewe wamelengwa kushambuliwa haki zao zimedhulumiwa katika nchi nyingi. Muungano wa EU huuamini kwamba ni muhimu kuhakikisha usalama na kutetea haki za wateteaji wa haki za binadamu. Kwa minajili hii ni muhimu kuangalia jambo la jinsia tunapoangazia jambo la wateteaji wa haki za binadamu.

## IV. MWONGOZO WA UTENDAJI KAZI

7. Njia mojawapo ya kufanya kazi ya Mwongozo inakusudiwa kutafuta njia zote za kufanya kazi katika kuendeleza na kuwalinda wateteaji wa haki za binadamu katika nchi, zinazoendelea katika Sera za Pamoja za Usalama.

### Kufuatilia na kutoa ripoti za ukadiriaji

8. Wakuu wa muungano wa EU wameshaombwa kutoa ripoti za mara kwa mara juu ya hali ya haki za binadamu katika nchi za uwakilishi. Baraza Linaloshughulikia Katika Haki za Binadamu (COHOM) limeidhinisha karatasi za maelezo ya ukweli ya kurahisisha kazi hii. Kufuatana na karatasi hizi na maelezo ya kweli, wakuu wa (misheni) ubalozi lazima waangazie hali ya wateteaji wa haki za binadamu katika ripoti zao, wakizingatia hasa vitisho vyovyote au kushambuliwa kwa wateteaji wa haki za binadamu. Katika hali hii wakuu (wa ubalozi) HoMs lazima wajue kwamba kiunzi cha kitaasisi chaweza kuwa na athari kubwa katika uwezo wa wateteaji wa haki za binadamu kwa kutekeleza kazi zao kwa usalama. Maswala kama bunge, mahakama, usimamizi au kutoa tahadhari (sheria) zinazochukuliwa na mataifa za kuwalinda waadhirika wa dhuluma zozote vitisho vya kulipiza kisasi upinzani au ubaguzi wa kisheria, kushirikizwa au tendo lolote la kiholela kama matokeo ya haki yake kutekeleza haki yoyote inayotajwa katika Daimio la UN kwa Wateteaji wa Haki za Binadamu ni muhimu katika jambo hili. Kunapohitajika wakuu wa ubalozi lazima watoe mapendekezo kwa (COHOM) kuwezesha hatua za EU, pamoja na kulaani vitisho na mashambulizi dhidi ya wateteaji wa haki za binadamu na vile vile malalamishi na kusema hadharani pale ambapo wateteaji wa haki za binadamu wako hatarini. HoMs lazima pia kutoa ripoti juu ya hatua mwafaka kwa EU katika matokeo

yanayotakikana.

9. Ripoti za HoMs na habari muhimu zozote kama ripoti na mapendekezo kutoka Uwakilishi Maalum wa Katibu Mkuu wa Wateteaji wa Haki za Binadamu, Waandishi Maalum wa UN na Mashirika ya Mikataba pamoja na mashirika yasiyo ya serikali itawezesha COHOM na makundi yoyote yanayofanya kazi, kuangazia hali ambapo hatua za EU zinahitajika na kuamua hatua zinazohitajika au kutoa mapendekezo ya hatua kama hizo kwa baraza la PSC.

**Wajibu wa ubalozi wa EU katika kufadhili na kuwalinda wateteaji wa haki za binadamu**

10. Katika nchi nyingi zinazoendelea ubalozi wa EU (Balozi wa EU Mataifa Shirika na Wajumbe wa Tume ya Ulaya) ndiyo ya muhimu baina ya Muungano na Mataifa Shiriki na wateteaji wa haki za binadamu wakiwamo. Wana wajibu muhimu wa kutekeleza sera za EU za wateteaji wa haki za binadamu. Ubalozi wa EU lazima watafute njia za kutekeleza sera zinazolenga wateteaji wa haki za binadamu. Ni lazima pia wafahamu kuwa wakati mwingine hatua za EU zinaweza kusababisha vitisho au mashambulizi dhidi ya wateteaji wa haki za binadamu. Ni lazima hivyo basi washauriane na wateteaji wa haki za binadamu iwezekanavyo kufuatana na hatua zinazofikiriwa. Tahadhari balozi za EU inaweza kuchukua ni pamoja na:

- kuratibu na kishiriki habari za wateteaji wa haki za binadamu pamoja na wale wako hatarini;
- kuendelea kuwa na mawasiliano mwafaka ya wateteaji wa haki za binadamu, pamojana kuwapokea Ubalozini na Kuwatembelea katika sehemu zao za kazi, itakuwa vizurikuwateua maafisa wa ushirikiano ikiwezekana katika kusaidiana mzigo wa hii kazi;
- kwa kutoa, utambulizi wa wateteaji wa haki za binadamu, panapofaa kwa njia za kutangaza, kuwatembelea au kuwakaribisha;
- kuhudhuria na kuchuunguza panapofaa, kutoa hukumu kwa wateteaji wa haki za binadamu.

**Kufadhili za wateteaji wa haki za binadamu kufuatana na nchi zinazoendelea na mikutano ya kimataifa ya wahusika.**

11. Lengo la muungano wa EU ni kuzishawishi nchi zinazoendelea kutekeleza majukumu yao kuziheshimu haki za wateteaji haki na kuwalinda kutokana na mashambulizi na vitisho kutoka kwa wahusika wasiyotoka serikalini. Katika kuwasiliana na nchi zinazoedelea muungano wa EU utaonelea kuwa muhimu, wa nchi zote kufuata na kuzingatia maadili ya viwango vya kimataifa hasa yale ya Daimio la UN. Lengo kuu zaidi ni lile la kuleta mazingira ambayo wateteaji wa haki za binadamu waweza kufanya kazi wakiwa huru. Muungano wa EU utatangaza malengo yake yajulikane kama sehemu yake muhimu ya sera zake za haki za binadamu na utaangazia umuhimu unayo kwa uteteaji wa wateteaji haki za binadamu. Hatua za kufadhili malengo haya ni pamoja na:

- kule ambako urais, au Uwakilishaji Mkuu wa CFSP au Wakilishaji Maalum na Mabalozi au Jumuiya ya Yuropa inatembelea nchi ambapo ikiwezekana kujumuisha kukutana na kuinua viwango vya wateteaji binafsi wa haki za binadamu kama sehemu muhimu ya kutembelea nchi zinazoendelea.
- sehemu ya haki za binadamu ya majadiliano ya kisiasa baina ya EU na nchi zinazoendelea, na mashirika ya kimaeneo, yatajumuisha hali ya wateteaji wa haki za binadamu ikiwezekana. Muungano wa EU utatoa ufadhili wake kwa wateteaji wa hakiza binadamu na kazi zao na kuinua viwango binafsi vinavyohusishwa ikiwezekana.
- kufanya kazi kwa karibu sana na nchi zenye mawazo kama hayo hasa katika Tume ya UN ya Uteteaji wa Binadamu na Makao Makuu ya UN.
- kufadhili na kuimarisha mikakati ya kimaeneo iliyomo ya kuwalinda wateteaji wa haki za binadamu kama kiini muhimu kwa wateteaji wa haki za binadamu wa Tume ya Ubinadamu na Watu Katika Haki na Kitengo cha Wateteaji Ndani ya Tume ya kimarekani katika haki za binadamu na kuazisha mikakati muhimu katika maeneo ambako hakuna.

**Ufadhili wa Utaratibu Maalum wa Tume ya UN ya Haki za Binadamu, pamoja na Uwakilishaji Maalum wa Wateteaji wa Haki za Binadamu**

12. Muungano wa EU unatambua kwamba Utaratibu wa Tume ya Haki za Binadamu, (Waandishi Maalum, Wawakilishaji Maalum, Wataalam Huru na Makundi Yafanyayo Kazi) ni muhimu katika bidii za kimataifa za kulinda wateteaji haki za binadamu kwa sababu ya uhuru wao na kutopendelea; uwezo wao kuchukua hatua na kuzungumzia dhuluma dhidi ya wateteaji wa haki za

binadamu duniani kote na kuzitembelea nchi. Huku Uwakilishaji wa Wateteaji Haki za Binadamu una jukumu muhimu katika jambo hili na mamlaka ya Utaratibu Maalum mwingineo ni wa muhimu pia kwa wateteaji wa haki za binadamu. Hatua za EU kwa kufadhili taratibu maalum zinajumuisha:

- kuhimiza mataifa yakubali kama njia moja kuu ya maombi ya kutembelea nchi katika taratibu maalum kwa UN;
- kufadhili kwa kupitia Ubalozi wa EU, matumizi ya kiini cha UN na mashirika ya kijamiiya haki za binadamu, jamii na wateteaji wa haki za binadamu pamoja na lakini bila kiwango kurahisisha kuanzisha mawasiliano na kubadilishana habari baina ya mikakati ya kiini na ile ya wateteaji haki za binadamu.
- kwa vile Taratibu Muhimu haziwezi kutekeleza mamlaka yao kwa kukosa rasilimali za kutosha, nchi shiriki za EU zitafadhili kwa kutoa hela za kutosha kutoka kwa makadirio ya kijumla katika Afisi ya Balozi Mkuu wa Haki za Binadamu.

**Kuwafadhili wateteaji wa Haki za Binadamu kwa njia za busara pamoja na Sera za Kimaendeleo.**

13. Mipangilio ya Muungano wa Ulaya na Mataifa Shiriki inayolenga kusaidia maendeleo ya kidemokrasia na taasisi, na kwa kukuza na kulinda wateteaji wa haki za binadamu katika mataifa yanayoendelea ni moja wapo ya njia pana na wazi za kuwasaidia wateteaji wa haki za binadamu. Hizi zaweza kuwa pamoja na lakini bila kikomo katika maendeleo. Ushirikiano wa mipangilio ya Washiriki wa Serikali. Ufadhili wa kibusara wajumlisha yafuatayo:

- mapatano baina ya nchi mbili ya haki za binadamu na mipango ya kidemokrasia na taasisi za kuwafadhili na kuwalinda wateteaji wa haki za binadamu katika mataifa yanayoendelea kwa njia ya mambo ya kuwafadhili wateteaji wa haki za binadamu kupitia kwa mambo kama yale ya kukuza uwezo na kufahamisha umma kwa njia za kampeni.
- kwa kuhimiza na kufadhili na kuimarisha kazi ya mashirika ya kitaifa ya kukuza na kutetea haki za binadamu, zilizowekwa kulingana na kanuni pamoja na taasisi za kitaifa za haki za binadamu, Ofisi ya Ufadhili na Tume za Haki ya Binadamu.
- kusaidia kwa kuanzisha mitandao ya wateteaji wa haki za binadamu katika viwango vya kimataifa pamoja na kuongoza mikutano ya wateteaji wa haki za binadamu;
- kwa kutafuta kuhakisha kwamba wateteaji wa haki za binadamu katika mataifa yanayoendelea yanaweza kufikia rasilimali pamoja na fedha (hela) kutoka ng’ambo(ulaya);

- kwa kuhakikisha kwamba mipango ya mafunzo ya haki za binadamu inafadhili mikutano ya haki za binadamu inafadhili mikutano baina ya UN Daimio juu ya Wateteaji wa Haki za Binadamu.

***Jukumu la Baraza la Kufanya Kazi kwa Makundi***

Kuambatana na mamlaka yake COHOM itaendelea kukagua utekelezaji na kufuatilia Miongozo ya Wateteaji wa Haki za Binadamu ikiongozwa kushirikiana pamoja na mabaraza mengine yafaayo kufanya kazi. Haya ni pamoja na:

- kukuza kufungamanishwa swala la wateteaji wa haki za binadamu katika sera na hatuazinazofaa za muungano wa EU.
- kufuatilia utekelezaji wa Miongozo katika nyakati zinazofaa;
- kuendelea kuchunguza inavyofaa, njia zaidi za ushirikiano na UN na mashirika mengine ya kimataifa na mikakati ya haki za binadamu.
- Kutoa ripoti kwa baraza kupitia, PSC na COREPER, inavyofaa katika kila mwisho wa mwaka juu ya mafanikio yanayafanywa katika kutekeleza Miongoz

**Kiambatisho cha I Kuambatisha Kiambatisho**

**Azimio la haki na wajibu a watu binafsi, makundi na vyombo vya jamii kwa kufadhili na kulinda kijumla haki ya binadamu inayotambulika na msingi wa uhuru**

**Bunge,**

**Kuthibitisha *umuhimu wa kuzingatia malengo na kanuni za haki za binadamu za umoja wa mataifa kwa ufadhili na ulinzi wa haki zote za binadamu na msingi wa uhuru kwa watu wote kati nchi zote za ulimwengu,***

*Kuthibitisha upya pia* umuhimu wa azimio la kijumla kwa haki za binadamu za pili na mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu kama maswala ya kimsingi ya bidii za kimataifa ya kufadhili heshima (hadhi) kwa wote na kufuata haki za binadamu na msingi wa uhuru na umuhimu kwa vyombo vingine vinavyochukuliwa ndani ya msingi ya umoja wa mataifa na pamoja na yale yaliopo kwenye viwango vya maeneo,

*Kusizitisha* kwamba wanachama wote wa umoja wa kimataifa utatekeleza kwa pamoja na kwa utengemano, jukumu lao la dhati kwa kufadhili na kuhimiza hadhi/heshima kwa haki za binadamu kwa msingi wa uhuru kwa wote bila tofauti zozote, pamoja na tofauti za kijinsia, kabila, rangi, lugha, dini, siasa au mawazo tofauti, kitaifa au msingi wa kijamii, mali, kuzaliwa au hadhi nyingineyo, na kuitikia upya umuhimu wa kufikia ushirikiano wa kimataifa kwa kutekeleza jukumu hili kulingana na hati ya haki za binadadamu.

*Kukubali* dhima muhimu ya ushirikiano wa kimataifa kwa, na kazi ya thamani ya watu binafsi, makundi na mashirika kwa kuchangia kwa, kuondoa kamili dhuluma zote za haki za binadamu na msingi wa uhuru wa watu na watu binafsi, pamoja kuhusu umma, dhuluma za wazi au za mipangilio kama zile za kiubaguzi wa rangi, aina zote za utenganisha wa kimbari, ukoloni, kuingiliwa na nchi za kigeni au kutwaaliwa, uingiliaji au matishio ya enzi za kitaifa, umoja wa kitaifa, uadilifu wa taifa na kutokubali kutambua haki za watu kujiamulia na haki za kila watu kutumia mamlaka kamili kuhusu mali yao na maliasili,

*Kukubali* uhusiano kati ya amani na usalama wa kimataifa ridhaa za haki za binadamu na msingi wa uhuru, na kujali kwamba kutokuwa na amani na usalama wa kimataifa hausingizii kutoafikiana,

*Kurudia kusema* kwamba haki zote za binadamu na msingi wa uhuru ni kwa wote, hazigawanyiki, za kutegemeana na ni zakuhusisha na zafaa zikuzwe na kutekelezwa kwa njia ya haki na usawa bila kuleta madhara kwa utekelezaji wa kila haki na uhuru hizo,

*Kusisitiza* kwamba jukumu kuu na wajibu wa kukuza na kuhifadhi haki za binadamu na msingi wa uhuru ni kazi ya serikali,

*Kukubali* haki na jukumu la watu binafsi, makundi na mashirika kukuza heshima na kulea fahamu za haki za binadamu na msingi wa uhuru kwa kiwango cha kitaifa na kimataifa.

*Kuazimia:*

*Ibara Ya Kwanza*

Kila mtu ana haki, binafsi na kwa ushirikiano na wengine, kukuza na kujitahidi kwa uhifadhi na uwezekano wa haki za binadamu na msingi wa uhuru kwa kiwango cha kitaifa.

*Ibara Ya Pili*

1. Kila taifa lina jukumu kuu na wajibu wa kuhifadhi, kukuza na kutekeleza haki zote za binadamu na msingi wa uhuru, pamoja na mambo mengine, kwa kuazimia hatua zinazofaa kuleta hali unaofaa kwa kijamii, kisiasa, na kwingineko, na pia hakikisho za kisheria zinazohitajika kuhakikisha kwamba kila watu walio chini ya utekelezaji wa sheria, binafsi na kwa ushirikiano na wengine, wanaweza kufurahi haki hizo zote za uhuru ziliko.

2. Kila serikali itaazimia sheria hizo, usimamizi na hatua zinazofaa kuhakikisha kwamba haki na uhuru zinazotajwa katika Azimio la sasa zahakikishiwa vikamilifu.

*Ibara Ya Tatu*

Sheria za kindani zilizolingana na Mkataba wa Umoja wa Mataifa na majukumu mengine ya kimataifa ya serikali kuhusu haki za binadamu na msingi wa uhuru ndiyo mifumo ya kisheria ambazo haki za binadamu na msingi wa uhuru wafaa kutekelezwa na kufurahiwa na ndizo juhudi zinazotajwa katika Azimio la sasa kwa kukuza, kuhifadhi na utekelezaji kamilifu za haki na uhuru hizo vipasavyo.

*Ibara Ya Nne*

Hakuna lolote katika Azimio la sasa litakalo onekana kudhoofisha azma na maadili ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa au kama kuzuia au kupungunza kutoka utoaji wa Mkataba wa Haki za Binadamu Kwa Wote, Mapatano ya Haki za Binadamu ya Kimataifa na vyombo vya kimataifa na wajibu ya kimataifa katika shughuli hizi.

*Ibara Ya Tano*

Kwa azma ya kukuza na kuhifadhi haki za binadamu na msingi wa uhuru, kila mmoja ana haki; binafsi na kwa ushirikiano na wengine, kwa kiwango cha kitaifa na kimataifa:

(a) Kukutana au kusanyika kwa amani;

(b) Kuanzisha, kujiunga na kushiriki katika mashirika yasiyo ya serikali, mashirika au makundi:

(c) Kuwasiliana na mashirika yasiyo ya serikali / mashirika ya serikali.

*Ibara Ya Sita*

Kila mmoja ana haki, binafsi na kwa ushirikiano na wengine;

(a) Kujua, kuuliza, kupata, kupokea na kuwa na habari kuhusu haki zote za binadamu na msingi wa uhuru, pamoja na kuwa na uwezo wa kupata habari jinsi haki na uhuru hizo zimepewa uwezo katika mfumo wa baraza la sheria za kindani, mfumo wa

mahakama au mfumo wa utawala;

(b) Vilivyo kwa haki za binadamu na vyombo vingine vya kimataifa vinavyohusika, kwa uhuru kuchapisha, kuarifu au kueneza kwa wengine fikira, habari na elimu zote za haki za binadamu na msingi wa uhuru;

(c) Kujifunza, kujadili, kuanzisha na kuwa na dhana kwa kufuata, zote mbili kwa sheria na kwa desturi za haki zote za binadamu na msingi wa uhuru na kwa njia hizi na zingine zinazofaa kujulisha kwa umma mambo haya.

*Ibara Ya Saba*

Kila mmoja ana haki, binafsi na kwa ushirikiano na wengine, kuanzisha na kujadili mawazo na maadili mapya ya haki za binadamu na kutetea zikubaliwe.

*Ibara Ya Nane*

1. Kila mmoja ana haki; binafsi na kwa ushirikiano na wengine, kuwa na uwezo kamili bila ubaguzi wowote ule kufikia, kushiriki katika serikali yake au ya nchi yake na katika shughuli zake za umma.

2. Haya yanahusisha, pamoja na mambo mengine, haki, binafsi na kwa ushirikiano na wengine, kutii idara za serikali na ajenti na mashirika yanayohusika kukosoa shughuli za umma na kutoa mapendekezo kwa ajili ya kuboresha hali zao na kudokeza mswada wowote unaoweza kuzuia au kudhoofisha kukuza, kuhifadhi na kufualu kwa haki za binadamu na msingi wa uhuru.

*Ibara Ya Tisa*

1. Katika shughuli za haki za binadamu na msingi wa uhuru, pamoja na kukuza na kuhifadhi haki za binadamu zilizotajwa katika Azimio la sasa, kila mmoja ana haki, binafsi na kwa ushirikiano na wengine, kunufaika kwa suluhisho kamili na kulindwa panapo dhuluma za haki hizo.

2. Kwa hiyo, kila mmoja ambaye haki au uhuru wake unadhulumiwa ana haki, aidha binafsi au kuwakilishwa halali, kutoa lalama kwa mahakama na kuhakikisha kwamba lalama hilo lichunguzwe mara moja hadharani mbele ya mahakama huru, bila

mapendeleo na yenye uwezo au baraza lolote liloanzishwa na sheria na kupata uamuzi kamili kutoka kwao kisheria, kutoa suluhu, na kutoa ridhaa zilizoko, panapo dhuluma kwa haki au uhuru wa mtu huyo, na pia kutekeleza uamuzi na fidia zote bila kusita.

3. Vile vile, kila mmoja ana haki, binafsi na kwa ushirikiano na wengine, pamoja na mambo mengine:
   (a) Kulalamikia sera na utekelezaji wa ofisa binafsi na idara za serikali kuhusu dhuluma za haki za binadamu na msingi wa uhuru, kwa maombi au kwa njia inayofaa, kwa mahakama ya kindani yenye uwezo, kwa idara za utawala zenye uwezo, au baraza la sheria lenye uwezo au idara yoyote yenye uwezo iliyoidhinishwa na mfumo wa sheria za Taifa, ambazo zitekeleze uwamuzi wao kuhusu lalama bila kusita.
   (b) Kuhudhuria vikao vya umma, kusikizwa kwa kesi na mashtaka ili kujiamulia kwa kulingana na sheria za kitaifa na wajibu na msimamo wa kimataifa unaotumika;
   (c) Kutoa huduma wa usaidizi wa kitaluma za kisheria au ushauri wowote unaofaa na kusaidia kutetea haki za binadamu na msingi wa uhuru.

4. Vile vile, na kulingana na vyombo vya kimataifa na sera za kimataifa zinazotumika, kila mmoja ana haki, binafsi, na kwa ushirikiano na wengine, uwezo wa kufikia bila kikwazo na kuwasiliana na mashirika ya kimataifa yaliyo na uwezo wa kawaida au uwezo maalumu kupokea na kuzingatia mawasiliano kuhusu mambo ya haki za binadamu na msingi wa uhuru.

5. Serikali itafanya uchunguzi usio na mapendeleo mara moja au kuhakikisha kwamba uchunguzi unafanyika panapo sababu za kuamini kwamba dhuluma za haki za binadamu na msingi wa uhuru umefanyika katika sehemu ya enzi yoyote iliyo chini ya utekelezaji wa sheria zake.

*Ibara Ya Kumi*

Hakuna atakayeshiriki, kwa matendo au kwa kutotenda kunapohitajika kudhulumu haki za binadamu na msingi wa uhuru na hakuna atakayeadhibiwa au kuchukuliwa hatua yoyote kwa kukataa kufanya hivyo.

| *Ibara Ya Kumi Na Moja* |
|---|
| Kila mmoja ana haki, binafsi na kwa ushirikiano na wengine, kushughulikia kazi yake au taaluma yake kisheria. Kila mmoja ambaye, kwa sababu ya kazi yake, anaweza kuathiri utu wa mtu, haki za binadamu na msingi wa uhuru wa wengine anafaa kutekeleza haki hizo na kuzingatia hali za ubora na kanuni na maadili ya kitaifa na kimataifa ya kazi. |
| *Ibara Ya Kumi Na Mbili* |
| 1. Kila mmoja ana haki, binafsi na kwa ushirikiano na wengine, kushiriki katika harakati za amani dhidi ya dhuluma ya haki za binadamu na msingi wa uhuru.<br><br>2. Serikali itahakikisha imechukua hatua zote kamili zinazofaa kulinda kila mmoja, binafsi na kwa ushirikiano na wengine, dhidi ua vurugu yoyote, tisho lolote, kisasi, ubaguzi wa bila kupinga au ubaguzi mkali wa kisheria, shirikizo au tendo lolote litokealo kwa matendo halali kwa haki zinazotajwa katika Azimio la sasa.<br><br>3. Kufuatia haya, kila mmoja ana haki, binafsi na kwa ushirikiano na wengine, kulindwa vikamilifu kufuatia sheria za kitaifa wanapopinga au kukataa, kwa njia za amani, shughuli na matendo, pamoja na kutotenda, yanayohusu serikali yanayogusia dhuluma za haki za binadamu na msingi wa uhuru, pamoja na matendo ya vurugu yanayofanywa na makundi au binafsi yanayoathiri furaha za haki za binadamu na msingi wa uhuru. |
| *Ibara Ya Kumi Na Tatu* |
| Kila mmoja ana haki, binafsi na kwa ushirikiano na wengine, kuomba, kupokea na kutumia mali na nguvu kwa azma ya kukuza na kuhifadhi haki za binadamu na msingi wa uhuru kwa njia za amani, kwa kulingana na ibara ya tatu ya Azimio la sasa. |
| *Ibara Ya Kumi Na Nne* |
| 1. Serikali ina jukumu la kuchukua hatua kupitia baraza la sheria, mahakama, idara za utawala au hatua yoyote inayofaa kukuza ufahamu wao wa haki zao za kiuraia, kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa watu wote walio chini ya utekelezaji wa sheria zake.<br><br>2. Hatua nazo zitakua, pamoja na mambo mengine:<br><br>(a) Uchapishaji na kusambaza sheria za kitaifa zilizoko na taratibu na msingi wa vyombo vya |

haki za binadamu za kimataifa zinazotumika;

(b) Uwezo wote kamili kwa wote wa kufikia nyaraka za kimataifa kuhusu haki za binadamu, pamoja na ripoti za serikali za mara kwa mara kwa vikundi thabiti vilivyoanzishwa na maafikiano yahaki za binadamu za kimataifa ambayo serikari ni mwanachama, pia pamoja na nyaraka kwa ufupi za majadiliano na ripoti rasmi za vikundi hivi.

3. Serikali itahakikisha na kusaidia, panapowezekana kuanzisha na kustawisha zaidi taasisi huru kukuza na kuhifadhi haki za binadamu na msingi wa uhuru katika enzi yote iliyo chini ya utekelezaji wa sheria zake, aidha wawe wachungunzi maalumu, tume ya haki za binadamu au taasisi yoyote ya kitaifa.

*Ibara Ya Kumi Na Tano*

Serikali ina jukumu la kukuza na kurahisisha kuelimisha haki za binadamu na msingi wa uhuru katika viwango vyote vya elimu na kuhakikisha kwamba wanao jukumu la kuwafunza wanasheria, watunza sheria/polisi, wanajeshi, watumishi wa umma pamoja na asili zifao za haki za binadamu katika mpango wa mafunzo yao.

*Ibara Ya Kumi Na Sita*

Watu binafsi, mashirika yasio ya serikali na taasisi husika wana dhima ya kuchangia kwa kujulisha umma maswala yote yanayohusu haki za binadamu na msingi wa uhuru kupitia shughuli kama vile elimu, mafunzo na utafiti kuimarisha maswala haya, pamoja na mambo mengine, kufahamu, uvimulivu, amani na uhusiano mwema kati ya mataifa na kati ya makabila yote na makundi ya kidini kwa kutia maanani asili ya jamii na jumia wanayotumia kutekeleza shughuli zao.

*Ibara Ya Kumi Na Saba*

Katika shughuli za haki na uhuru zilizotajwa katika Azimio la sasa, kila mmoja, akitenda binafsi na kwa ushirikiano na wengine, watafuatilia tu kwa kuligana na wajibu wa msimamo wa kimataifa unaotumika na unaamuliwa tu na sheria kwa azma ya utambuzi na heshima kwa haki na uhuru wa wengine na kufikia mahitaji halali ya uadilifu, wema wa umma na ustawi wa kawaida katika jamii yenye demokrasia.

*Ibara Ya Kumi Na Nane*

1. Kila mmoja ana wajibu kwa na katika jamii, na ndiye pekee anayeweza kustawisha nafsi yake kwa uhuru na vikamilifu.

2. Watu binafsi, makundi, taasisi na mashirika yasiyo ya serikali wana dhima ya kutekeleza na jukumu kwa kuhifadhi demokrasia, kukuza haki za binadamu na msingi wa uhuru na kuchangia kukuza na maendeleo ya jamii yenye demokrasia, taasisi na namna.

3. Watu binafsi, makundi, taasisi na mashirika yasiyo ya serikali pia wana dhima na jukumu kwa kuchangia, vifaao, kwa kukuza haki za kila mmoja kwa kijamii na hali ya kimataifa ambako haki na uhuru zilizowekwa mbele katika Mkataba wa Haki za Binadamu Kwa Wote na vyombo vingine vya haki za binadamu vinaweza kutimizwa vikamilifu.

*Ibara Ya Kumi Na Tisa*

Hakuna lolote katika Azimio la sasa litakalo chukuliwa kuwa la mtu wowote binafsi, kundi au sehemu yoyote ya jamii au serikali yoyote, haki ya kuwa na shughuli yoyote au kutenda jambo lolote linalo kusudi kwa uharibifu wa haki na uhuru zilizotajwa katika Azimio la sasa.

*Ibara Ya Ishirini*

Hakuna lolote katika Azimio la sasa litakalo chukuliwa kuruhusu serikali kuunga mkono na kukuza shughuli za watu binafsi, makundi ya watu binafsi, taasisi au mashirika yasioyo ya serikali kinyume cha kanuni za Mkataba wa Umoja wa Mataifa.

***Kiambatisho II kwa Kiambatisho kwa KIAMBATISHO***

Vyombo vifaavyo vya kimataifa

- Azimio la Haki za Binadamu Kwa Wote
- Mapatano ya Kimataifa kuhusu Haki za Uraia na Kisiasa.
- Mapatano ya Kimataifa kuhusu Haki za Kiuchumi, Jamii na Utamaduni
- Makubaliano ya kupinga Mateso na Ukatili wowote, Unyama au Tendo la Kuvunja Heshima au Adhabu.
- Makubaliano kuhusu Haki za Watoto.
- Makubaliano kuhusu Kumaliza Ubaguzi wa Wanawake.
- Makubaliano kuhusu Kumaliza aina zote za Ubaguzi wa Kimbari.

- Makubaliano ya Bara Ulaya kuhusu Haki za Binadamu, hati zake za awali na kesi za sheria husika za mahakama ya Bara Ulaya kwa Haki za Binadamu.
- Mkataba wa Jamii ya Ulaya/Mkataba Mpya wa Jamii ya Ulaya.
- Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Haki za watu.
- Makubaliano ya Marekani kuhusu Haki za Binadamu.
- Makubaliano ya Geneva kuhusu Kulinda Waathiriwa wa Vita na Hati zake za Awali na pia sheria za kimila kwa wanadamu zinazotumika wakati wa mapigano.
- Makubaliano ya Mwaka wa 1951 kuhusu Hali ya wakimbizi na Hati zake za Awali za Mwaka wa 1967.
- Amri za Roma ya Mahakama ya Jinai ya Kimataifa.
- Azimio kuhusu Haki na Jukumu ya Watu Binafsi, Makundi na Mifumo ya Jamii kukuza na kuhifadhi kwa wote Haki za Binadamu na Msingi wa Uhuru unaojulikana.